# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kutokana na Janga la Corona (COVID-19) Nchini na Duniani kwa ujumla, napenda kuwataarifu wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa kuwa; maambukizi ya COVID-19 kwa sasa yako ndani ya nchi tofauti na hapo awali ambapo Maambukizi yalikuwa yanaletwa kutoka Nchi ambazo zimeathirika kwa kiasi kikubwa. Maambukizi ya sasa ni kutoka kwenye baadhi ya Maeneo yalioathirika ndani ya Nchi na kusambaa kwenye Mikoa mingine.

Kutokana na hali hii, natoa maelekezo kwa wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa kuwa:-

1. Abiria wote wanaoingia ndani ya Mkoa wa Rukwa kutokea Mikoa mingine watatakiwa kupimwa Afya zao kwa Kipima Joto (Thermal scanner) kwenye Vituo vya Laela na Namanyere. Aidha, wakifika kwenye Kituo Kikuu cha mabasi cha Sumbawanga watatakiwa kupimwa pia. Hali kadhalika, abiria wote wanaoingia Mkoa wa Rukwa wanashauriwa kuvaa Barakoa.

2. Abiria wanaoingia Mkoa wa Rukwa kutoka kwenye Maeneo yaliyoathirika wanashauriwa kujitenga wao wenyewe kwa hiari yao kwa muda wa Siku Kumi na Nne (14). Endapo watahisi au kugundua kuwa wanaona dalili zozote za matatizo ya kiafya watatakiwa kuripoti kwenye Kituo chochote cha Afya cha karibu.

3. Wafanyabiashara wote ndani ya Mkoa wanashauriwa kuagiza bidhaa kwa njia ya simu na kulipa kupitia Benki badala ya wao kusafiri. Kwa wafanyabiashara wadogo wanahimizwa kuagiza bidhaa kwa pamoja ili kuwa na urahisi kupata usafiri wa pamoja.

4. Wamiliki wa Nyumba za Kulala Wageni na Hoteli zote wanatakiwa kusimamia uandikaji wa taarifa za Wageni kwa umakini kwa ajili ya kuwatambua kwa urahisi. Taratibu zote za kuandika taarifa za Wageni zifuatwe. Wageni wote watakiwe kufuata Maelekezo ya Wataalam wa Afya ikiwa ni pamoja na kuvaa Barakoa.

5. Wahudumu wote wa Nyumba za Kulala Wageni na Hoteli wachukue tahadhari ya kulinda Afya zao kwa kuvaa Barakoa pamoja na kufuata maelekezo yote ya Wataalam wa Afya.

6. Watu wote wanaofanya kazi za kutoa huduma kwenye Maduka, Maeneo yote ya Kuuza vyakula, Saluni, Super Market n.k. wanatakiwa kuvaa Barakoa.

7. Wananchi wote wakiwemo wanafunzi waache safari zisizo kuwa za lazima watulie majumbani au kuendelea na shughuli zao huku wakizingatia maelekezo muhimu ya Wataalam wa Afya juu ya kujikinga na COVID-19.

8. Familia zinapotaka kufanya manunuzi ya jumla (sokoni na kwingineko), inashauriwa aende mtu mmoja tu kutoka kila familia kufanya manunuzi hayo. Hata kwenda Hospitali kuona

Wagonjwa anatakiwa aende mtu mmoja tu. Aidha, Mwanafamilia husika anayetoka nyumbani asisahau kuvaa Barakoa.

9. Wakurugenzi wa Halmashauri zote (Sumbawanga, Kalambo, Nkasi na Manispaa ya Sumbawanga) wanatakiwa kuhakikisha kuwa Minada yote na Magulio inadhibitiwa na kuendeshwa kulingana na Maelekezo ya Wataalam wa Afya na Serikali kwa Ujumla. Kinyume na hapo Serikali ya Mkoa haitasita kusitisha Mnada / Gulio husika (kwa muda hadi watakapojipanga vizuri) pale itakapobainika kuwa kuna ukiukwaji wa taratibu na maelekezo ya Wataalam / Serikali. Kila Mnada utafuatiliwa kulingana na tarehe ya kufanyika kwa mnada huo.

10. Baa zote, Vilabu vya Pombe na Night Clubs zinatakiwa kuendeshwa kwa mujibu wa Leseni za Biashara kwa kuzingatia maelekezo ya Wataalamu wa Afya. Wamiliki wa Baa na Vilabu watatumiwa Maelekezo Mahsusi juu ya kutekeleza maelekezo ya Wataalam / Serikali na kusimamiwa kupitia Serikali za Mitaa na Vijiji/Vitongoji.

Nasisitiza kuwa kila Mtu atekeleze maelekezo haya kwa usalama wa Afya zetu.

JOACHIM L. WANGABO
**MKUU WA MKOA**
**RUKWA**
**20 Aprili, 2020**